JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA
(BaruazotezipelekwekwaMkurugenziwaManispaa)

MKOA WA TABORA
SIMU : 026-2604316/2606088
FAX: 026 2604835

S. L. P. 174,
TABORA -TANZANIA

20/09/2019

TANGAZO

MAELEKEZO YA UCHAGUZI

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kwa Mamlaka aliyopewa chini ya kanuni ya 9 (1), (2) **ya kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa Katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019** kama zilivyotangazwa na Gazeti la Serikali Namba 372 la tarehe 26/04/2019, na kanuni ya 9 (1), (2) **ya kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijij, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019** kama zilivyotangazwa na Gazeti la Serikali Namba 374 la tarehe 26/04/2019, anatoa maelekezo ya uchaguzi kwamba uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 utafanyika tarehe 24 Novemba 2019, nafasi zitakazo gombewa ni pamjoa na Menyekiti wa Mtaa, Wajumbe wa Kamati ya Mtaa, Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, na Wajumbe wa Halmashuri ya Kijiji. Jedwali Namba 1 hapa chini linatoa muhutasari wa maelekezo ya uchaguzi:-

Jedwali Na 1 Maelekezo ya Uchaguzi.

Na	Tukio	Maelekezo
1	Tarehe ya Kufanyika kwa Uchaguzi.	Uchaguzi Utafanyika Tarehe 24/11/2019
2	Muda na Sehemu ya Kuandikisha Wapiga Kura.	Vituo vya kuandikisha wapiga kura vitakuwa maeneo yaliyoteuliwa katika Mtaa na Kitongoji husika, na vitafunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa Kumi na mbili kamili Jioni.

3	Muda na mahali pa kufanyia uchaguzi	Zoezi la upigaji kura litaanza saa mbili kamili asubuhi na kumalizika saa kumi kamili jioni, na upigaji kura utafanyika katika kituo ambacho mpiga kura alijiandikisha.
4	Sifa za Mpiga Kura	Ili mtu awe na sifa ya kupiga kura ni lazima awe na sifa zifuatazo:- ➢ Awe raia wa Tanzania ➢ Awe na umri wa miaka 18 au zaidi ➢ Awe ni mkazi wa eneo la Mtaa, au Kitongoji kusika ➢ Awe hana ugonjwa wa akiri ambao uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya utabibu. ➢ Awe amejiandikisha kupiga kura katika Mtaa au Kitongoji husika.
5	Sifa za Mgombea katika nafasi za Mwenyekiti wa Mtaa, Wajumbe wa kamati ya Mtaa Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji.	Mtu yeyote anayetaka kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa Mtaa, Mjumbe wa Kamati ya Mtaa, Mwenyekiti wa Kijiji, Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji, ni lazima awe na sifa zifuatazo:- ➢ Awe ni raia wa Tanzania ➢ Awe na umri wa miaka 21 au zaidi ➢ Awe na uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au kiingereza. ➢ Awe na shughuli halali ya kumwezesha kuishi ➢ Awe mkazi wa Mtaa, Kijiji au Kitongoji husika ➢ Awe mwanachama wa chama cha Siasa na adhaminiwe na Chama hicho ➢ Awe hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabala ya tarehe ya uchaguzi. ➢ Awe hana ugonjwa wa akiri ambao uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya utabibu.
6	Fomu za Kugombea nafasi za Mwenyekiti wa Mtaa, Wajumbe wa kamati ya Mtaa Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji.	Fomu za kugombea zitapatikana katika Ofisi za Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakayekuwa katika ofisi za Kata, Mitaa, na Vijiji husika.
7	Muda wa Kuchukua na	Fomu zitatolewa kuanzia saa moja na nusu

	kurejesha Fomu za Kugombea nafasi za Mwenyekiti wa Mtaa, Wajumbe wa kamati ya Mtaa Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji.	asubuhi. Na zitatolewa kuanzia tarehe 29/10/2019 hadi tarehe 04/11/2019. **Mwisho wa kurejesha fomu utakuwa ni tarehe 04/11/2019 saa kumi kamili jioni.**
8	Uteuzi wa wagombea	Uteuzi wa wagombea kwa nafasi za Mwenyekiti wa Mtaa, Wajumbe wa Kamati ya Mtaa, Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji utafanyika tarehe 05/11/2019. Majina ya wagombea walioteuliwa yatabandikwa katika ofisi za Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi zilizopo katika ofisi za kata, mitaa na vijiji.
9	Muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi	Mapingamizi kuhusu uteuzi yatawasilishwa kuanzia tarehe 05-06/11.2019 ambapo mtu yeyote aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kuwasilisha pingamizi na kumwomba Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi uliofanyika, na pingamizi hili litatakiwa liwasilishwe ndani ya siku mbili tangu uteuzi ulipofanyika. Mgombea ambaye hata ridhika na uamuzi wa Msimaizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye kamati ya rufaa katika muda usiozidi siku nne kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimaizi wa Uchaguzi.
11	Tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi	Rufaa zitawasilishwa na kusikilizwa kuanzia tarehe 05-08/11/2019 Kamati ya rufaa itatoa uamuzi wa rufaa ndani ya muda wa siku nne kuanzia siku ya kupokea rufaa na uamuzi wake utakuwa wa mwisho. Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa kamati ya rufaa atakuwa na haki ya kufungua shauri katika mahakama ya Wilaya ndani ya siku 30 baada ya matokea ya uchaguzi kutangazwa.
12	Kipindi cha kuendesha	➢ Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia

	Kampeni za Uchaguzi	tarehe 17-23/11/2019, ➢ Zitafanyika kwa muda wa siku 7, ➢ Kila chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitatakiwa kuwasilisha ratiba ya kampeni kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku saba kabla ya muda wa kampeni kuanza ➢ Mikutano ya kampeni za Uchaguzi kwa mujibu wa ratiba iliyopitishwa na kuwasilishwa kwa Mkuu wa Polisi Wilaya itaanza saa mbili kamili asubuhi na kumalizika saa kumi na mbili kamili jioni. ➢ Endapo mgombea au Chama Cha Siasa chenye mgombea kitakusudia kufanya mabadiliko ya ratiba ya mikutano ya kampeni, mgombea au Chama hicho kitafanya hivyo baada ya kuwasilisha kwa maandishi mapendekezo ya mabadiliko hayo Kwa Msimamizi wa Uchaguzi na mapendekezo hayo kujadiliwa na kuridhiwa na vyama vima vinavyoshiriki uchaguzi, na mabadiliko hayo kuwasilishwa kwa Mkuu wa Polisi kwa ajili ya kupewa ulinzi.

Maelekezo haya yametolewa leo tarehe 23/09/2019

William D. Mpangala
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
MANISPAA YA TABORA.

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA